# TAARIFA YA MWENYEKITI

**MKUTANO MKUU WA MWAKA WA NNE WA WANAHISA**
**TAREHE 29 AGOSTI 2016**

Mabibi na Mabwana,

Kwaniaba ya Bodi ya Wakurugenzi wa Precision Air, napenda kuwakaribisha wote kwenye mkutano mkuu wa nne (4) wa wanahisa. Leo nitawasilisha kwenu ripoti za kampuni kwa mwaka ulioshia tarehe 31 Machi 2014 na tarehe 31 Machi 2015.

Kabla ya kuanza, napaenda kuchukua nafasi hii kuwatambulisha wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ambao wapo hapa nasi siku ya leo. Kwa kuanzia kulia;

- Mr. Mbuvi Ngunze - Mjumbe
- Mr. Vincent Shirima - Mjumbe
- Mr. Ron Schipper - Mjumbe
- M/s Elizabeth Minde - Mjumbe
- M/s Sauda Rajab - Mjumbe
- Mr. Migire Migire - Kaimu Katibu wa Kampuni

Hayati Nelson Mandela aliwahi kusema "Mara zote jambo huonekana haliwezekani, mpaka linapofanyika" usemi huu unashahabiana na hali ya Precision Air, kwani miaka michache iliyopita wakati tunaianza safari ya changamoto, wengi waliamini kampuni hii ingekufa, lakini leo hii bado tupo imara na tunashuhudia tukipiga hatua kubwa katika harakati za kuleta mabadiliko katika kampuni hii.

Leo nnaposimama mbele yenu, tunashuhudia mafanikio katika kupungua kwa hasara ya uendeshaji kwa kiwango cha asilimia 52 kwa mwaka wetu wa fedha wa 2015-16 pamoja na mazingira magumu ya biashara. Kwa mwaka jana hasara ya uendeshaji ilikua Shilingi za Kitanzania Bilioni 53, Lakini kwa mwaka huu hasara hiyo imepungua hadi Bilioni 25. Hii ni ishara ya kwamba hatuko mbali na tunapotamani kufika. Ikumbukwe kwamba kwa mwaka 2013-2014 kampuni ilipata faida ya uendeshaji ya Shilingi bilioni 3.

Mafanikio ya mwaka huu wa fedha yamepatikana kutokana na mafanikio katika utekelezwaji wa mpango mkakati wa kuleta mageuzi katika kampuni uliotangazwa mwaka uliopita.
Hatua madhubuti za ubanaji matumizi, kukua kwa mapato ya ziada (ambayo kwa mwaka huu yamekua kwa asilimia 100) ni moja ya mambo makuu yaliyochangia kupungua kwa hasara ya uendeshaji kwa kiwango cha shilingi Bilioni 28.

Kwa upande mwingine, Mauzo ya kampuni yalishuka kwa kiwango cha asilimia 16, kwani shirika liliweka sokoni siti 311,213 kwa kilometa, ikilinganishwa na siti 323,000 kwa kilometa zilizowekwa sokoni kwa mwaka jana ambazo zilikua ni pungufu kwa asilimia 64 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2013-14.

Matokea ya mwaka huu, yamechagizwa na shirika kuwa na idadi ndogo ya ndege kwa ajili ya shughuli za shirika, ambapo hali hiyo ilisababishwa na injini 13 kuwa katika matengenezo makubwa. Hili, pamoja na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Kitanzania, bei za mafuta zisizo tabirika pamoja hali tete yaa usalama katika ukanda wa Afrika Mashariki, vimepelekea shirika kupata hasara kabla ya kodi ya Shilingi za Kitanzania bilioni 91.6, ikiwa ni ongezeko la asilimia 12 ikilinganishwa na hasara ya mwaka jana ya Shilingi Bilioni 83 ikiwa ni ongezeko la asilimia 14 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2013-14.

Kuporomoka kwa kiwango cha siti Milioni 11 kwa kilometa (ASK), kulikosababishwa na upungufu wa ndege kufuatia injini kuwa katika ukarabati mkubwa, kumechangia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa faida kabla ya makato kwa kiwango cha asilimia 37% hadi Bilioni 19.4. Katika mwendelezo huo tumeshuhudia kushuka kwa idadi ya abiria kwa kiwango cha asilimia 17 na kuathiri wastani wa kujaa kwa ndege kwa asilimia 9.

Mtakumbaka kwenye mkutano wa mwisho kama huu tuliwaalezea matarajio yetu ya kukamilisha mpango wa kuuza na kuzikodisha ndege zetu (sale and lease back) ambapo mpango huu ungetuwezesha kujiweka katika hali bora kimtaji, mpaka sasa tunasikitika mpango huo haujakamilika lakini tumefikia katika hatua nzuri. Kuchelewa kwa mpango huu kumesababishwa na taratibu za uthibitishwaji wa mpango huu kwa serekali za Ufaransa, Italia, Finland na Canada. Hatahivyo tayari serekali za nchi hizo zimeshatoa baraka zao na upembuzi yakinifu umeshaanza. Matarajio ni kukamilisha mchakato huu mwishoni mwa mwaka huu.

**Mikakati**

Shirika limedhamiria kuendelea na jitihada za kujiimarisha kifedha kwa kuongeza uzalishaji wa mapato and kuendelea na jitihada za kubana matumizi.

Shirika litaweka kipaombele katika maeneo yafuatayo;

- Kupitia upya mtandao wetu wa safari na kupanga upya njia zetu za safari ili kuhakikisha yakua huduma tunayotoa sokoni inaendana na mahitaji ya wateja wetu.

- Kuendeleza na kuimarisha ushirikiano na mashirika ya Ndege ya kimataifa pamoja na mshirka wetu shirika la Ndege la Kenya na kuhakikisha tunafaidika na biashara ya kuunganisha abiria wakimataifa. Hili litatuwezesha kuimarisha nafasi yetu katika soko la abiria kimataifa.
- Shirikia pia litaendela na jitihada za kusimamia matumizi kikamilifu na kuhakikisha linabana matumizi na kuepuka matumizi yasiokua na tija. Tumefanya vyema mwaka huu katika eneo hili na tunaamini tutaweza kufanya vyema zaidi.
- Kwa mwaka huu wa fedha 2015-16 tumeshuhudia mapato ya ziada yakikua kwa asilimia zaidi ya 100. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na biashara ya kukodi ndege zetu , kutoa huduma ya matengenezo ya ndege kwa mashirika mengine pamoja na maeneo mengine . Tunatarajia kukuza mapato yetu ya ziada kwa kuongeza juhudi katika ukodishaji wa ndege kwani mpaka sasa kumeonyesha kuwa na faida.
- Uongozi wa shirika pia utaendelea na jitihada za kufufua ndege zetu zilizo kuwa chini kwaajili ya matengenezo na kuhakikisha zinarudi kufanya safari ili tuweze kuongeza uwezo wa kuzalisha mapato na hatimaye kuzalisha faida.
- Tutajikita pia katika jitihada za kulipa madeni yetu na kuhakikisha linakua katika kiwango kinacho endena na uwezo wetu wa kulipa na kwa kufanya hivyo tutawavutia wawekezaji kuja na kuwekeza fedha zao kwenye shirika letu.
- Vile vile sshirika litaendelea na juhudi za kutafuta wawekezaji, wakuja kuwekeza katika shirika letu na kuimarisha mtaji wetu hivyo kutupa nguvu yakutoa ushindani katika soko la ndani na kikanda pia.

Wachumi wanamsemo unaosema “ Kama mambo yatabaki kama yalivyo” shirika linatarajia kushuhudia matunda ya mpango wa mageuzi na uwezeano wa kutangaza faida kwa mwaka wa fedha 2016/17 kama mipango yote itatekelezwa kikamilifu.

Tunaendelea kuwaomba ushirikiano wenu kama wanahisa na mabalozi wetu katika jamii yetu, katika kuendelea kulitangaza shirika lenu sokoni kwa ujumla na kupitia hilo kulisaidia shirika kuongeza idadi ya abiria wanaosafiri nasi na kuhakikisha tunafanikisha mageuzi ya shirika letu.

Baada ya kuyasema hayo, nasikitika kutangaza kuwa shirika haliko katika nafasi ya kutoa gawiwo kwa mwaka huu wa fedha.

Shirika litaendelea na jitihada za kuboresha utendaji katika biashara ili kuongeza uzalishaji wa mapato na kuimarisha upatikanaji wa fedha za uendeshaji wa shughuli za shirika. Kama nilivyoeleza hapo awali ni matarajio ya shirika kupata faida kwa mwaka 2016/17.

Nashukuru kwa usikivu wenu.

- MWISHO -